Ujasiri Wa Kuhubiri Injili
(Boldness To Preach The Gospel)

Na

Alex S. Silvester

Ujasiri Wa Kuhubiri Injili
(Boldness To Preach The Gospel)

Na

Alex S. Silvester

Oktoba 11, 2018

Ujasiri Wa Kuhubiri Injili

Watu wengi wanadhani kwambaa mafundisho ya uongo yanaweza kwenda nje kirahisi na kwa mara moja, lakini mitume wasingefanya hivyo kwa saa moja. Tunapaswa kuonyesha ujasiri wa hali ya juu tunapokabiliana na mafundisho ya uongo pale ambapo dalili zake hutokea.

Yerusalemu yote ilikuwa kwenye taharuki wakati uongozi wa Kiyahudi walipofikiria kwamba kumwua Yesu kungeleta hitimisho wa mafundisho yake na umaarufu uliokuwa unasababishwa miongoni mwa watu. Siku tatu kufuatia kuzikwa kwa Yesu, mwili wake ulikosekana kwenye kaburi na Yerusalemu yote ilifahamu. Na malaika wakawatokea wanawake fulani akieleza, "*Hayupo hapa kwani amefufuka kama alivyosema. Njooni mpatazame mahali alipolazwa.*" (Mat. 28:6). Wale waliotilia mashaka kufufuka kwa Yesu walidhani Wakristo wamekosea wakipeleka nyumbani kwao kwamba kifo cha Kristo pale Kalvari ilikuwa dhabihu kwa ajili ya dhambi. Ukuu wa Kristo ulidhibitishwa pale ambapo mwili wa Yesu ulipofufuliwa siku ya tatu (Mdo. 2).

Mahakama ya Kiyahudi kingewatarajia Petro, Yakobo, Yohana na mitume wengine kuogopa kutokana na vitisho vyao. Lakini nafahamu kwamba hiyo isingekuwa sababu hata kidogo, kama hofu yao ya awali ilibadilishwa na kuwa na ujasiri. Paulo anasema, "*Kama vile nilivyotarajia sana, na kutumaini, kwamba sitaaibika kamwe, bali kwa uthabiti wote kama siku zote na sasa vivyo hivyo Kristo ataadhimishwa katika mwili wangu; ikiwa kwa maisha yangu, au ikiwa kwa mauti yangu.*" (Fil. 1:20). Lugha halisi inapendekeza kwamba, "Jaribu kufanya, au kufanya kitu kibaya au kigumu; au kuvumiliana na mtu kwa ujasiri, shughulika kwa ujasiri." Wakristo wa kwanza walikuwa na ujasiri katika kazi zao ili kumtukuza Kristo. Baraza la wazee lilimtishia Petro na Yohana waache kuhubiri katika jina la Yesu Kristo na majibu yao yalikuwa, "*Maana sisi hatuwezi kuacha kuayanena mambo tuliyoyaona na kuyasikia.*" (Mdo. 4:20). Kama tunahitaji kumtumikia Kristo leo, tunapaswa kufanya hivyo kwa ujarisiri waliokuwa na Wakristo wa karne ya kwanza.

- **Tunahitaji ujasiri kuwahubiria wasioamini.** Hapo mwanzo nimeeleza kwamba mitume walikuwa katika majaribu na wazee wa baraza. Kanisa likakuwa kwa haraka kufikia wanaume 5000, bila kuwahesabu wanawake na watoto. Naamini kwamba wengine wamekadiria kanisa kuwa na watu 20000 -25000 kwa wakati huu. Wazee wa baraza walichukia na kutaka kuvuruga ukuaji huo wa haraka, na mitume wawili waliombwa kutoa kutoa majibu ya miujiza na ukuaji wa kanisa uliokuwa unatokea. Petro alisema

kwamba ilikuwa ni kwa mamlaka au uwezo wa Yesu Kristo kwamba haya yote yamepita (Mdo. 4:10-12). Ujumbe huu wa "njia pekee" haukutengenezwa ili kuwafanya maarufu; hataivyo ingehitaji, uvumilivu na ujasiri ili iweze kuwa na nguvu (Mdo. 4:13). Moja ya hitaji katika siku zetu ni kuwashawishi watu kwamba wamepotea dhambini (Rum. 3:23; Eze. 18:20). Zaidi na zaidi mimbari hushinda kwa nguvu ya Injili (Rum. 1:16). Pia ninaamini kwamba dozi ya saikolojia na mifumo mingine hutolewa kama changamoto wakati nafsi za wanadamu hufupishwa kwa ujumbe wenye nguvu wa Kristo (Yoh. 14:6; 1 Pet. 4:11; Heb. 4:12). Tunapaswa kuonyesha kwa roho ya upendo na upole jinsi gani dhambi ilivyo mbaya na kwamba siku ya hukumu inawasubiri wale wanaokataa ujumbe wa Injili (Marko 16:16; Gal. 1:8-9).

- **Tunahitaji kuwa na ujasiri kukabiliana na mafundisho ya uongo.** Kuwakemea wale wanaofundisha uongo siyo rahisi, hataivyo, Yesu alifanya hivyo ilipohitajika. Yesu aliwaambia Masadukayo na Mafarisayo, "*Watu hawa huniheshimu kwa midomo ila mioyo yao iko mbali nami. Nao waniabudu bure, wakifundisha mafundisho yaliyo maagizo ya wanadamu.*" (Mat. 15:8-9). Kwa baadhi miongoni mwa Wayahudi hao Yesu alisema, "*Ninyi ni wa bab yenu Ibilisi na tamaa za baba yenu ndizo mpendazo kuzitenda. Yeye alikuwa mwuaji tangu mwanzo; wala hakusimama katika kweli, kwa kuwa hamna hiyo kweli ndani yake. Asemapo uongo asema yaliyo yake mwenyewe, kwa sababu yeye ni mwongo na baba wa huo.*" (Yoh. 8:44). Yesu hakuangalia njia nyingine alipowaona Mafarisayo wakengeufu wakifundisha mafundisho ya wanadamu kwa sheria ya Mungu. Mitume walionyesha ujarisiri mkuu walipokuwa wanakabiliana na ukengeufu wa kidini. Wakati wengine walipojaribu kufunga Agano la Kale kwa Wakristo walioishi wakati ule, Paulo alipinga. "*Ambao hata saa moja hatukujitia chini yao, ili kwamba kweli ya Injili ikae pamoja nanyi.*" (Gal. 2:5). Tunaishi katika siku za uhuru naa ruhusa ya kidini wakati kila kitu kina kwenda. Yamkini Paulo hakuwa wa ushawishi huu asingeweza kukubaliana na upotofu wa kidini. "*hakuna, hakuna hata kwa saa moja."* Zaidi sana wengi wanaweza kutoa mafundisho ya uongo na kukaa wakidhani kwamba wamemaliza.

- **Tunahitaji ujasiri katika kuhubiri kweli yote.** Mara nyingi kuna majaribu kuhubiri kile ambacho watu wanataka kusikia, kuliko wanachohitaji kusikia. Fikiria kwamba daktari wako anasema, "yote ni sawa," wakati mwili wako umejaa Malaria au ugongojwa

mwingine unaoua. Tungependa daktari wetu awe anakuja na kutoa matibabu kamili naa mwongozo ambao utapelekea kupona. "*Kwa maana watu hawa ni watu waasi, watoto wasemao uongo, watoto wwasiotaka kuisikia sheria ya BWANA; wawaambiapo waonaji, msione, na manabii msitoe unabii, wa mambo ya haki, tuambieni maneno laini, hubirini maneno yadanganyayo.*" (Isa. 30:9-10). Israeli waliwakataa manabii na kukataa "mambo mazuri" wakitarajia kile kilichowadanganya. Ni jinsi gani mifumo iliyokuwepo kipindi cha Isaya inavyofanana na hali ya sasa katika karne hii.

Tuangalie mtazamo ulioelezwa na Paulo, "*Kwa maana sikujiepusha na kuwahubiria habari ya kusudi lote la Mungu.*" (Mdo. 20:27). Inahitaji ujasiri wa hali ya juu kuhubiri kweli yote, hasa tukijua ya kwamba baadhi hawataikubali. Tunapaswa kuhubiri kweli yote ya imani inayookoa, kanisa moja, ubatizo kwa ajili ya ondoleo la dhambi, ibada inayokubalika, vyombo vya mziki, talaka na ndoa, matumizi ya vikombe vingi katika ibada na wale waliozianzisha, na masomo mengi muhimu. Hatuwezi kubadilisha injili ili kutimiza mahitaji ya mwanadamu wa leo. Mwandishi wa Waebrania alihitimisha na ukweli thabiti, "*Yesu Kristo ni yule yule jana leo na hata milele.*" (Heb. 13:8). Neno ambalo lingefuata: kama Yesu Kristo ni yule yule jana, leo, na milele je hatupaswi kuhitimisha kwamba Neno hili ni lile lile jana, leo, na milele? Mtazamo wa kila Mkristo unapaswa kuwa "*kusema kweli kwa upendo.*" (Efe. 4:15).

Na huu ndio wajibu wetu kuhakikisha kwamba inasikilizwa duniani kote.

Alex Sadat Silvester